**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

---

# RATIBA YA SHUGHULI ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE KUANZIA TAREHE 03 HADI 23 AGOSTI, 2026

---


Idara ya Kamati za Bunge,
Ofisi ya Bunge,
10 Barabara ya Morogoro,
S.L.P 941
40490 Tambukareli,
**DODOMA**

**YALIYOMO**

**1.0 UTANGULIZI ... ii**

1.1 Maelezo ya Jumla ... ii

1.2 Shughuli Zilizopangwa ... ii

1.1.1 Kuchambua Miswada ya Sheria ... ii

1.1.2 Kuchambua Sheria Ndogo ... iii

1.1.3 Kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2024/25 ... iii

1.1.4 Kupokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ... iii

**2.0 RATIBA YA KILA KAMATI YA KISEKTA ... 1**

2.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria ... 1

2.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo ... 4

2.3 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama ... 7

2.4 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ... 10

2.5 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii ... 13

2.6 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira ... 22

2.7 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo ... 24

2.8 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii ... 27

2.9 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI ... 32

2.10 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu ... 35

2.11 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Nishati na Madini ... 39

**3.0 RATIBA YA KILA KAMATI YA SEKTA MTAMBUKA ... 42**

3.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo ... 42

3.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ... 45

**4.0 RATIBA YA KILA KAMATI INAYOSIMAMIA MATUMIZI YA FEDHA ZA UMMA ... 48**

4.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ... 48

4.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) ... 53

**RATIBA YA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE KUANZIA**
**TAREHE 03 HADI 23 AGOSTI, 2026**

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Maelezo ya Jumla

Mkutano wa Nne wa Bunge utaanza siku ya Jumanne, tarehe 25 Agosti, 2026. Kama ilivyo ada, Mkutano huo utatanguliwa na Vikao vya Kamati za Kudumu za Bunge kumi na sita (16), ambapo Kamati nne (04) zitatangulia kuanza vikao tarehe 03 Agosti, 2026 na Kamati kumi na mbili (12) zitaanza vikao tarehe 10 Agosti, 2026. Kamati zitakazotangulia ni:

(i) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo;

(ii) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC);

(iii) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC); na

(iv) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC).

Kamati hizo hutangulia kutokana na utaratibu wa Bunge kutekeleza wajibu wake wa kufuatilia utekelezaji wa madaraka yake ya kutunga sheria yaliyokabidhiwa serikalini, mahitaji ya Kamati kuhusu muda wa uchambuzi wa Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na utekelezaji wa jukumu la Bunge kufuatilia uwekezaji wa mitaji ya umma (Public Investment) kupitia Kamati ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC).

Kamati kumi na mbili (12) zilizosalia zitaanza vikao tarehe 10 Agosti, 2026. Vikao vya Kamati zote kumi na sita (16) zitakamilika ifikapo tarehe 23 Agosti, 2026

### 1.2 Shughuli Zilizopangwa

Shughuli za Kamati katika kipindi hicho zinajumuisha maandalizi ya shughuli za Mkutano wa Nne wa Bunge na shughuli nyingine za ufuatiliaji na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za umma kama ifuatavyo: -

#### 1.1.1 Kuchambua Miswada ya Sheria

Shughuli hii inatokana na miswada mitatu ya Sheria kupelekwa kwenye Kamati mbili kwa mujibu wa kanuni ya 100(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025. Miswada hiyo iliyosomwa Mara ya Kwanza tarehe 26 Juni, 2026 ilipelekwa kwenye Kamati zifuatazo:

(i) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria iliyopelekewa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 02) wa mwaka 2026; na

(ii) Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo iliyopelekewa miswada miwili (2): Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kilimo wa Mwaka 2026 [The Agricultural

(Amendments) Bill, 2026] na Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.

### 1.1.2 Kuchambua Sheria Ndogo

Sheria ndogo zilizowasilishwa katika Mkutano wa Tatu wa Bunge zitachambuliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Shughuli hiyo imepangwa kufanyika kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge za Mwaka 2025.

### 1.1.3 Kupokea na Kujadili Taarifa Mbalimbali za Utendaji wa Serikali na Taasisi zake

Kamati kumi na moja za kisekta zitapokea na kujadili taarifa mbalimbali za utendaji wa Serikali na Taasisi zake. Shughuli hii imepangwa kwa mujibu wa kifungu cha 7(c) na (d) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Aidha, Kamati ya Bajeti itapokea na kujadili taarifa mbalimbali kutoka Serikalini kwa lengo la kutekeleza jukumu lake la kusimamia, kuchambua, kuratibu na kulishauri Bunge kuhusu sera za fedha za umma, mapato ya Serikali, Bajeti ya Serikali na Mpango wa Maendeleo wa Taifa.

### 1.1.4 Kuchambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Kuhusu Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka 2024/25

Kamati mbili za kusimamia Matumizi ya Fedha za Umma zitachambua Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu hesabu zilizokaguliwa za wizara, taasisi, mashirika ya umma na Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2025. Shughuli hii imepangwa ili kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma kwa mujibu wa kifungu cha 13, Kifungu cha 14 na kifungu cha 15 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge. Kamati zinazohusika ni Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) na Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC).

### 1.1.5 Kupokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) itapokea na kuchambua Taarifa za Uwekezaji wa Mitaji ya Umma ili kubaini iwapo uwekezaji huo una ufanisi na kuwa umezingatia taratibu na miongozo mujarabu ya biashara. Shughuli hii itafanyika kwa mujibu wa kifungu cha 11(1) na (2) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

## 2.0 RATIBA YA KILA KAMATI YA KISEKTA

### 2.1 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria

**Ukumbi**: Frank Mfundo - Ghorofa ya 5, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala;<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026;<br>☞ Kupokea maelezo ya jumla ya Sekretarieti kuhusu dhana kuu katika Maudhui ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026); na<br>☞ Kupokea uchambuzi wa kisheria kuhusu Ibara za Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026); na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (SBUU) kuhusu hatua iliyofikiwa katika kutatua changamoto za Udhibiti wa Dawa za Kulevya nchini zilizoainishwa katika ripoti ya hali ya Dawa za Kulevya nchini ya mwaka 2025. | ☞ Wajumbe<br>☞ AG<br>☞ WN–OWM (SBUU) |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kusikiliza na kupokea maoni ya wadau kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026); na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MUUUB) kuhusu utendaji wa Tume ya Utumishi wa Umma katika taasisi za umma ili kubaini uzingatiaji wa sheria, ufanisi wa Tume hiyo katika kushughulikia rufaa na malalamiko kutoka kwa watumishi wa umma na mamlaka mbalimbali za ajira pamoja na ufuatiliaji wa rufaa hizo zinazoenda katika ngazi za juu ikiwemo mahakama. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MUUUB |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kuchambua maoni yaliyokusanywa kutoka kwa Wadau na majumuisho ya Hoja zote zilizojitokeza ili kupata Jedwali la uchambuzi na Hoja zinazohitaji ufafanuzi wa Serikali; na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MUUUB) kuhusu usimamizi na ushughulikiaji wa maadili ya Viongozi wa Umma ikiwemo uhakiki wa uzingatiaji wa ahadi za uadilifu, tamko la mali na madeni na ushughulikiaji wa malalamiko na mashauri: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MUUUB |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kukabidhi Serikalini Jedwali la Hoja zitokanazo na Uchambuzi na majumuisho ya Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026;<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya mchakato wa ukamilishaji wa awamu ya Nne ya Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF): Matarajio na hatua za utekelezaji wake; na<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya ukamilishaji wa Rasimu ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MUUUB |
| **J'mosi & J'pili**<br>15&16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais (MU) kuhusu -<br>(i) mikakati ya kuhakikisha kwamba Sera, Sheria na Kanuni zinaendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 kabla na baada ya kuanza utekelezaji wake: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) usimamizi wa uandaaji, utekelezaji na usimamiaji wa bajeti za Mapato na Matumizi kwa mashirika ya umma yasiyotegemea Bajeti ya Serikali Kuu: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MU |
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Katiba na Sheria kuhusu uendeshaji wa mashauri ya Wanawake, Watoto na Watu wenye ulemavu katika vyombo vya upatikanaji haki nchini; na<br>☞ Kushauriana na Serikali kuhusu Hoja zitokanazo na Uchambuzi wa Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026*). | ☞ Wajumbe<br>☞ WKS<br>☞ AG<br>☞ MMM |
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kukamilisha mashauriano Kuhusu marekebisho ya Sheria ya Kuzuia Utakatishaji wa Fedha Haramu | ☞ Wajumbe<br>☞ AG |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
| --- | --- | --- |
| | yanayopendekezwa katika Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2026. | |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa kuhusu uandaaji wa Mpango Mkakati wa maeneo maalumu ya kiuchumi yaliyotengwa kwa muda mrefu bila kuendelezwa na hatua zilizofikiwa katika ulipaji wa fidia kwa wananchi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR-MU |
| | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM) Kuhusu Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uchumi wa Buluu: Mipango, mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Kupitia rasimu ya Taarifa ya Maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2) wa Mwaka 2026 (The Written Laws (Miscellaneous Amendments) (No. 2) Bill, 2026). | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22&23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WN-OWM (SBUU)** = Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Uratibu na Wenye Ulemavu)
- ☞ **WN-OR (MUUUB)** = Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora)
- ☞ **WN-OR (MU)** = Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Mipango na Uwekezaji)
- ☞ **WN-OMR (MM)** = Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira)
- ☞ **WKS** = Waziri wa Katiba na Sheria
- ☞ **MMM**= Mtendaji Mkuu wa Mahakama
- ☞ **AG** = Mwanasheria Mkuu wa Serikali

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (hardcopy) mbili (2) tu na nakalatepe (Soft Copy) ziwasilishwe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.2 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo

**Ukumbi:** Msekwa D, Jengo la Pius Msekwa

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala;<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026; na<br>☞ Kupokea maelezo ya jumla ya Sekretarieti kuhusu dhana kuu na uchambuzi wa kisheria kuhusu -<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea Maelezo ya Waziri wa Kilimo kuhusu -<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kusikiliza na kupokea Maoni ya wadau kuhusu -<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026 | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kusikiliza na kupokea Maoni ya wadau kuhusu -<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kuchambua maoni yaliyokusanywa kutoka kwa Wadau na majumuisho ya Hoja zote zilizojitokeza ili kupata Jedwali la uchambuzi na Hoja zinazohitaji ufafanuzi wa | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
| --- | --- | --- |
| | Serikali na Kuwasilisha Serikalini Jedwali la Hoja zitokanazo na Uchambuzi na majumuisho. | |
| **Jumamosi**<br>15 Agosti, 2026 | ☞ Kukabidhi Serikalini Jedwali la Hoja zitokanazo na Uchambuzi wa:<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026.<br>☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Kilimo kuhusu utendaji wa -<br>(i) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (NiRC): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) Bodi ya Tumbaku Tanzania: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) Bodi ya Pamba Tanzania: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumapili**<br>16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Kilimo kuhusu utendaji wa -<br>(i) Wakala wa Hifadhi ya Chakula ya Taifa (NFRA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) Kampuni ya Mbolea Tanzania (TFC): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania: (TFRA) Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Kilimo |
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kushauriana na Serikali kuhusu hoja zilizobainishwa katika jedwali la hoja zitokanazo na uchambuzi wa Miswada ya -<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. | ☞ Wajumbe<br>Waziri wa Kilimo |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utendaji wa -<br>(i) Wakala wa Usajili wa Biashara (BRELA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Tume ya Ushindani (FCC): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WVB |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utendaji wa -<br>(i) Shirika la Viwango Tanzania (TBS): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WVB |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhusu utendaji wa -<br>(i) Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) Bodi ya Nyama Tanzania (TMB): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) Bodi ya Maziwa Tanzania (TDB) Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMUV |
| **Jumamosi**<br>22 Agosti, 2026 | ☞ Kupitia Rasimu ya Taarifa ya Maoni ya Kamati kuhusu -<br>(i) Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria za Kilimo wa Mwaka 2026 (The Agricultural) (Amendments) Bill, 2026; na<br>(ii) Muswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto wa Mwaka 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumapili**<br>23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WVB** – Waziri wa Viwanda na Biashara
- ☞ **WMUV** – Waziri wa Mifugo na Uvuvi

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.3 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama

**Ukumbi:** Herman Serwat - Ghorofa ya 5, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wabunge kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa majukumu ya Kituo cha Uhusiano wa Kimataifa cha Dkt. Salim Ahmed Salim (SAS - CFR);<br>(ii) vigezo vinavyotumika kufungua maeneo ya uwakilishi/Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi pamoja na manufaa yanayotarajiwa; na<br>(iii) majukumu ya Balozi za Tanzania Nje ya Nchi, na namna zinavyochangia kutekeleza Diplomasia ya Uchumi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WNJE |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa majukumu ya Kituo cha Kimataifa cha Mikutano Arusha (AICC) pamoja na hali ya ukusanyaji wa madeni ambayo kituo kinadai kwa taasisi mbalimbali; na<br>(ii) utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kituo kipya cha kisasa cha mikutano cha Mount Kilimanjaro International Convention Centre (MK- ICC). | ☞ Wajumbe<br>☞ WNJE |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano wa ukarabati na uendelezaji wa milki katika Balozi za Tanzania Nje ya Nchi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) utekelezaji wa Mpango wa Hiari wa Afrika wa Kujitathmini katika Utawala Bora (APRM) kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WNJE |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa majukumu ya Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) mkakati wa kukamilisha ujenzi wa Nyumba 3,036 ambazo ni sehemu ya Nyumba 10,000 zilizokuwa zinajengwa kwa mkopo kutoka Jamhuri ya Watu wa China. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Ulinzi na JKT |
| **J'mosi & J'pili**<br>15&16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa majukumu ya Shirika la NYUMBU: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) utekelezaji wa majukumu ya Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Ulinzi na JKT |
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) hali ya wahamiaji haramu katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Julai, 2026: Mafanikio na changamoto za utaratibu wa VISA on Arrival; na<br>(iii) uhamiaji Mtandao katika Ofisi za Jeshi la Uhamiaji Nchini: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMNN |
| **Jumatano**<br>19 Agosti,2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu -<br>(i) hatua iliyofikiwa kwenye utekelezaji wa mpango wa kuwarejesha Wakimbizi katika nchi zao na utambuzi wa Wakimbizi waishio nje ya makambi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(ii) utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Msajili wa Jumuiya kwa kipindi cha Julai, 2025 hadi Julai, 2026: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi;<br>(iii) utatuzi wa migogoro ya ardhi baina ya Jeshi la Magereza na wananchi/taasisi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na | ☞ Wajumbe<br>☞ WMNN |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | (iv) utekelezaji wa majukumu ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuhusu -<br>(i) hali ya usalama wa raia na mali zao nchini katika kipindi cha Aprili hadi Juni, 2026;<br>(ii) mkakati endelevu wa kudhibiti ajali za barabarani nchini: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(iii) mkakati wa kukabiliana na makosa mapya ya kiuhalifu yanayotokana na maendeleo ya teknolojia: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMNN |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22&23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WMNN** – Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi
- ☞ **WNJE** – Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz.

## 2.4 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

**Ukumbi:** Anne Makinda - Ghorofa ya Tano, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) ukarabati wa barabara zilizoharibiwa na mvua za masika nchini;<br>(ii) maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya BRT; na<br>(iii) mpango wa kuboresha huduma za usafirishaji zinazotolewa na UDART. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) mikakati ya Serikali katika kulinda maeneo ya wazi katika miji, halmashauri, na majiji nchini; na<br>(ii) uendelezaji wa maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya bustani kwenye majiji nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu mkakati wa Wizara katika -<br>(i) ujenzi wa viwanja vya michezo kwenye shule za msingi na sekondari nchini; na<br>(ii) ajira za walimu wa michezo kwenye shule za msingi na sekondari nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu mkakati wa Wizara katika -<br>(i) uimarishaji wa huduma za maji kwenye shule za msingi na sekondari nchini;<br>(ii) upandaji wa miti na utunzaji wa mazingira kwenye shule za msingi na sekondari nchini; na<br>(iii) uimarishaji wa lishe katika shule za msingi nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **J'mosi & J'pili**<br>15&16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu - | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | (i) tathmini ya ujenzi wa shule za Sekondari za Wasichana za Mikoa; na<br>(ii) tathmini ya ujenzi wa shule za Sekondari za Wavulana za Kanda. | |
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa afua za viuadudu katika halmashauri nchini;<br>(ii) uzingatiaji wa agizo la Serikali katika utekelezaji wa afua za viuadudu kwenye halmashauri saba (7): Kinondoni – Dar es Salaam; Mkuranga – Pwani; Kilombero – Morogoro; Muleba – Kagera; Kakonko na Buhigwe – Kigoma; na Bunda – Mara. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI) kuhusu -<br>(i) ujenzi wa uzio kwa shule za Sekondari zilizo kwenye mazingira hatarishi nchini;<br>(ii) tathmini ya shule za bweni za sekondari nchini ambazo hazina mabwalo ya chakula na mpango wa Serikali wa ujenzi wa mabwalo hayo;<br>(iii) mahitaji ya walimu na hali ya upatikanaji wake katika kukidhi mabadiliko ya mtaala wa elimu nchini utakaoanza kutekelezwa 2028; na<br>(iv) mkakati wa upatikanaji wa vifaa vya kufundishia, kujifunzia kwa ajili ya madarasa hayo mawili (la sita na la saba) yatakayoanza kidato cha kwanza kwa pamoja mwaka 2028. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI)kuhusu -<br>(i) utendaji wa stendi za mikoa nchini;<br>(ii) hali ya changamoto ya magari kutokupita Stendi ya Mabasi ya Magufuli – Dar es Salaam: Athari zilizojitokeza na hatua za utatuzi wa changamoto hiyo; na<br>(iii) ufanisi wa Stendi sita za Mabasi ambazo ni: Stendi ya Magufuli – Dar es Salaam; Stendi ya Msamvu – Morogoro; Stendi ya Nanenane – Dodoma; Stendi ya Nyegezi – Mwanza; Stendi ya Nyamhongolo – Mwanza; na Stendi ya Mabasi ya Kange – Tanga. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (TAMISEMI) |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22 & 23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- **WN-OWM (TAMISEMI) –** Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
- **DART** – Dar es Salaam Rapid Transport
- **UDART –** UDA Rapid Transit Public Limited Company
- **BRT –** The Bus Rapid Transit

**TANBIHI:**

- Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.5 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii

**Ukumbi:** Mathias Kihaule - Ghorofa ya Tano, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026; | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu utekelezaji wa Programu ya Wanagenzi nchini: Mchango katika kukuza ujuzi, ajira na changamoto zinazojitokeza katika utekelezaji wake. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Usalama na Afya Mahali pa Kazi kwa kuzingatia -<br>(i) mwenendo wa usajili wa maeneo ya kazi na utoaji wa elimu kwa wadau; na<br>(ii) tathmini ya mwitikio wa waajiri na wafanyakazi pamoja na changamoto za usimamizi wa masuala hayo. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu -<br>(i) mwenendo wa utoaji wa huduma za fidia kwa wafanyakazi kupitia Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) ufanisi wa utoaji wa fidia na muda wa kushughulikia madai: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu (KAM) kuhusu mwenendo wa -<br>(i) uratibu wa zoezi la utambuzi, usajili na upangaji wa maeneo ya kazi kwa Watafuta kazi;<br>(ii) mchakato wa uratibu upatikanaji na usimamizi wa ajira za nje ya nchi; na<br>(iii) udhibiti na usimamizi wa vyombo vya ajira na ukusanyaji wa taarifa za soko la ajira. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OWM (KAM) |
| **J'mosi & J'pili**<br>15&16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuhusu hali ya utoaji wa huduma katika makazi ya wazee kwa kuzingatia upatikanaji wa huduma za msingi, miundombinu na rasilimali watu: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMJWM |
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu kuhusu mwenendo wa utoaji na urejeshaji wa mikopo inayotolewa kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMJWM |
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kuhusu uratibu na uendeshaji wa majukwaa ya vijana; Mchango wake katika ushiriki wa vijana kwenye maendeleo ya Taifa na changamoto zilizopo. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR (MV) |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Rais Maendeleo ya Vijana kuhusu utekelezaji wa programu za kuwawezesha vijana kiuchumi kwa kuzingatia -<br>(i) mwenendo wa utoaji na urejeshaji wa mikopo ya vijana;<br>(ii) aina za programu zinazotekelezwa na idadi ya wanufaika; na<br>(iii) mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OR (MV) |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22 & 23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WN –** Waziri wa Nchi
- ☞ **OWM –** Ofisi ya Waziri Mkuu
- ☞ **KAM –** Kazi, Ajira na Mahusiano
- ☞ **MV –** Maendeleo ya Vijana
- ☞ **WMJWM –** Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz.

### 2.6 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Maji na Mazingira

**Ukumbi:** Philip Marmo - Ghorofa ya Tano, Jengo Kuu la Utawala

| TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM) kuhusu biashara ya Hewa Ukaa nchini (Carbon Trade): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM)kuhusu -<br>(i) Mpango wa Taifa wa Kupambana na Kuenea kwa Hali ya Jangwa na Ukame (2025-2030); na<br>(ii) mkakati na hatua mahsusi katika kuimarisha usimamizi endelevu wa ardhi, kuhifadhi na kurejesha Uoto wa asili. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais (MM) kuhusu -<br>(i) mkakati na Mpango - kazi wa Taifa wa Uhifadhi wa Bioanuwai (National Biodiversity Strategy and Action Plan, NBSAP, 2025 - 2030); na<br>(ii) Mpango Mkakati wa Utoaji Elimu ya Mazingira kwa Umma. | ☞ Wajumbe<br>☞ WN-OMR-MM |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu -<br>(i) utekelezaji wa Miradi ya Maji (Gridi ya Taifa ya Maji); na<br>(ii) hatua iliyofikiwa kwenye ulipaji wa madeni ya Wakandarasi kwenye miradi ya maji nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **J’mosi &J’pili**<br>15&16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu kiasi cha fedha za Mfuko wa Maji kilichopokelewa kwa miaka mitatu 2024 hadi 2026 na mgawanyo wa fedha hizo kwa Mamlaka za Maji (RUWASA). | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |

| TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu mpango na mkakati wa kukabiliana na uchafuzi, uharibifu na uvamizi wa vyanzo vya maji. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu madeni sugu ya ankara za maji kwa taasisi za Serikali. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maji kuhusu -<br>(i) hali ya upatikanaji na usambazaji wa maji katika Jiji la Dodoma: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) hatua iliyofikiwa katika miradi ya ujenzi wa Mabwawa ya majitaka nchini. | ☞ Wajumbe<br>☞ Waziri wa Maji |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22 & 23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

☞ **WN-OMR-MM –** Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira

**TANBIHI:**

☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;

☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na

☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz.

## 2.7 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Elimu, Utamaduni na Michezo

**Ukumbi**: Namba. 49, Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex)

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu -<br>(i) hali ya upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia hususan vifaa vya amali na vitabu vya kiada ili kufikia uwiano wa kitabu kimoja mwanafunzi mmoja (1:1); na<br>(ii) mikakati ya kupunguza upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi na amali, wahadhiri na wakufunzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu -<br>(i) maendeleo ya ujenzi wa vyuo vya VETA 64 vya Wilaya na chuo cha VETA Mkoa wa Songwe; na<br>(ii) mkakati wa kuimarisha ubora wa mafunzo ya amali hususan elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi katika shule za sekondari na vyuo vya amali. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu -<br>(i) maendeleo ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Mwalimu Nyerere cha Kilimo na Teknolojia;<br>(ii) vigezo na upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu na vyuo vya kati;<br>(iii) mkakati wa kisayansi wa kujenga umahiri wa kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK); na<br>(iv) mkakati wa upatikanaji wa huduma ya utoaji wa chakula na lishe shuleni. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu -<br>(i) vigezo na upatikanaji wa mikopo ya elimu ya juu na vyuo vya kati; na<br>(ii) mkakati wa utekelezaji wa mpango wa ushirikiano kati ya taasisi za elimu ya juu (vyuo) na soko la ajira (viwanda na taasisi) mbalimbali. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **J'mosi & J'pili**<br>15 &16 Agosti,2026 | **MAPUMZIKO WA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti,2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu -<br>(i) maandalizi ya Mashindano ya Mpira wa Miguu kwa Timu za Taifa za Wanaume Afrika (AFCON 2027) na maendeleo ya ujenzi na ukarabati wa viwanja vitakavyotumika; na<br>(ii) kanzidata ya ajira katika sekta ya habari, utamaduni, sanaa na michezo. | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu mikakati ya -<br>(i) ujenzi wa arena ya michezo na sanaa eneo la Kawe - Dar es Salaam;<br>(ii) ujenzi wa miundombinu ya akademia ya michezo Malya;<br>(iii) hatua iliyofikiwa katika ujenzi wa vituo 28 vya kurusha matangazo ya redio yenye masafa ya FM; na<br>(iv) ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya michezo katika shule 56. | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Afya na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kuhusu utekelezaji wa ushauri uliotolewa na Kamati ya pamoja mwaka 2024 ikijumuisha -<br>(i) ushirikishwaji na utoaji wa elimu kwa wadau kuhusu mchakato wa uhuishaji wa mitaala na uwekaji wa vigezo vipya vya udahili kwa kada za afya katika vyuo vya kati vya afya;<br>(ii) Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) kutekeleza majukumu kwa mujibu wa sheria sura namba 129 ikiwemo majukumu iliyoyakasimu kwa Wizara ya Afya; na<br>(iii) uanzishwaji wa chombo mahususi cha usimamizi na uendeshaji wa vyuo vya kati vya afya vilivyo chini ya Wizara ya Afya ili kuwezesha uendeshaji bora wa mafunzo ya fani za kada ya afya. | ☞ Wajumbe<br>☞ WEST<br>☞ Waziri wa Afya<br>☞ APHECOT |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu -<br>(i) kukuza na kubidhaisha Kiswahili kitaifa na kimataifa; | ☞ Wajumbe<br>☞ WHUSM |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| | (ii) kukamilisha ujenzi wa jengo la Kiwanda cha uchapaji na ununuzi wa mitambo ya kisasa ya uchapaji (TSN);<br>(iii) kuimarisha utendaji kazi wa maafisa utamaduni na maafisa maendeleo ya michezo waliopo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu -TAMISEMI; na<br>(iv) maendeleo ya Mfuko wa Utamaduni hususan utoaji wa mikopo na uendeshaji wa Mfuko. | |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22 & 23 Agosti,2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WEST –** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia
- ☞ **WHUSM –** Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo
- ☞ **APHECOT –** Umoja wa Vyuo Binafsi vya Afya Tanzania

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.8 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Utalii

**Ukumbi:** Namba. 44, Jengo Dogo la Utawala (Utawala Annex)

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
| **Jumatatu**<br>10 Agosti, 2026 | ☞ Shughuli za Utawala; na<br>☞ Kupokea maelezo mafupi (briefing) ya Sekretarieti kuhusu shughuli za Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **Jumanne**<br>11 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu -<br>(i) utendaji na usimamizi wa watumishi wa kada ya ardhi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) hatua iliyofikiwa katika uanzishaji wa Kamisheni ya Ardhi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **Jumatano**<br>12 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu utendaji wa Mabaraza ya Ardhi: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **Alhamisi**<br>13 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu hali ya migogoro ya ardhi nchini: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **Ijumaa**<br>14 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kuhusu utendaji wa Chuo cha Ardhi Morogoro na Chuo cha Ardhi Tabora: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WANMM |
| **J'mosi & J'pili**<br>15&16 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |
| **Jumatatu**<br>17 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu -<br>(i) hali sekta ya wanyamapori nchini: Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) hali ya migogoro ya mipaka katika maeneo yaliyohifadhiwa na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumanne**<br>18 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu utendaji wa -<br>(i) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi; na<br>(ii) Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI): Mafanikio changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |
| **Jumatano**<br>19 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu utendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |
| **Alhamisi**<br>20 Agosti, 2026 | ☞ Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Maliasili na Utalii kuhusu utendaji wa Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA): Mafanikio, changamoto na hatua za utatuzi. | ☞ Wajumbe<br>☞ WMU |
| **Ijumaa**<br>21 Agosti, 2026 | Majumuisho ya shughuli zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia tarehe 10 hadi 23 Agosti, 2026. | ☞ Wajumbe<br>☞ Sekretarieti |
| **J'mosi & J'pili**<br>22&23 Agosti, 2026 | **MAPUMZIKO YA MWISHO WA JUMA** | **WAJUMBE** |

**VIFUPISHO:**

- ☞ **WANMM –** Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi
- ☞ **WMU –** Waziri wa Maliasili na Utalii

**TANBIHI:**

- ☞ Vikao vitaanza saa 3.00 Asubuhi;
- ☞ Taarifa zote ziwasilishwe Ofisi ya Bunge angalau siku tatu (3) kabla ya tarehe ya kikao kinachohusika; na
- ☞ Wizara/Taasisi inayohusika itawasilisha Ofisi ya Bunge nakalamango (*hardcopy*) mbili tu na nakalatepe *(Soft Copy)* ziwasilishwe kwa baruapepe kupitia anuani: kamati@bunge.go.tz

### 2.9 Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Afya na Masuala ya UKIMWI

**Ukumbi:** Namba 09, Jengo Kuu la Utawala

| SIKU/TAREHE | SHUGHULI | MHUSIKA |
|---|---|---|
| **Jumapili**<br>09 Agosti, 2026 | Wajumbe kuwasili Dodoma | Katibu wa Bunge |
